

Kanuni ya tabia kwa wanafunzi

Habari kwa wanafunzi na wazazi au walezi

Shule za umma za NSW zimejitolea kutoa mazingira salama, yenye kuunga mkono, na yenye kuitikia kwa kila mtu katika mipangilio mbalimbali. Tunafundisha na kuonyesha mifano ya tabia jumuiishi na salama tunazothamini kwa wanafunzi wetu.

Katika shule za umma za NSW wanafunzi wanatarajiwa, kwa uwezo wao wote:

- kuonyesha heshima kwa wanafunzi wengine, walimu wao na wafanyakazi wa shule na wanajamii
- kufuata sheria za shule na za darasa na kufuata maelekezo ya walimu wao
- kujitahidi kupata viwango vya juu vya kujifunza
- kutenda kwa adabu na heshima ambayo inawafanya wanajamii wote wa shule kuhisi kuthaminiwa, kujumuishwa na kuungwa mkono
- kutatua migogoro kwa heshima, utulivu na haki
- kukidhi sera iliyokubaliwa ya shule ya sare au kanuni ya mavazi
- kuhudhuria kila siku (isipokuwa imeruhusiwa kisheria)
- kuheshimu mali zote
- kuwa salama na kutokuwa na vurugu au kuleta silaha, dawa za kulevya, pombe, mivuto, sigara za kielektroniki au tumbaku shuleni kwetu
- kutomdhulumu, kumnyanyasa, kumtisha, au kumbagua mtu yeyote katika shule zetu.

Shule zinachukua hatua katika kukabiliana na tabia ambayo inadhuru binafsi au wengine au kwa mafanikio ya kufundisha na kujifunza kwa hali ya juu.

Wanafunzi wana haki ya:

- usalama shuleni
- kupata na kushiriki kikamilifu katika masomo yao
- kuheshimiwa na wanafunzi wengine, walimu na wafanyakazi wa shule
- kueleza maoni yao, kuweka malengo na kujitetea.

Mkuu wa shule na wafanyakazi wa shule, kwa kutumia uamuzi wao wa kitaalamu, wako katika nafasi nzuri zaidi ya kudumisha nidhamu na kutoa mazingira salama, ya kuunga mkono na yenye kuitikia ujifunzaji na kutekeleza hatua inayofaa wakati wanafunzi hawafikii matarajio haya.

Idara ina wajibu kwa utoaji wa mfumo wa sera na rasilimali kama taarifa za masuala ya kisheria, kuupata ushauri wa kitaalam, na mafunzo ya kitaaluma ili kuwaongoza wakuu na wafanyakazi wao katika kutekeleza uamuzi wao wa kitaaluma.

Katika muktadha huu, Serikali ya NSW na Idara ya Elimu zitaunga mkono mamlaka na hukumu ya wakuu wa shule na wafanyakazi wa shule katika ngazi ya mtaa.

Kanuni ya tabia kwa wanafunzi: Matendo ya wanafunzi

Kukuza ujumuishaji, kujifunza, ustawi na usalama wa wanafunzi wote wa shule za umma za NSW ni kipaumbele cha juu kwa Idara ya Elimu.

Tunatekeleza mbinu za kufundisha na kujifunza katika mipangilio mbalimbali ili kusaidia ukuzaji wa ujuzi unaohitajika na wanafunzi ili kufikia viwango vyetu vya juu vya tabia ya heshima, salama na inayohusika.

Ili kukidhi matarajio yaliyowekwa hapo juu, wanafunzi kwenye shule za umma za NSW, kwa kadiri ya uwezo wao, wanapaswa kutii kanuni zifuatazo.

Heshima

- Mtendeaneni kwa utu.
- Wasiliana na ishi kwa adabu.
- Tenda na fanya kazi kwa ushirikiano na wanafunzi wengine, walimu na wafanyakazi wa shule.
- Kuza mahusiano mazuri na yenye heshima.
- Tathmini maslahi, uwezo na utamaduni wa wengine.
- Heshimu mahitaji ya kujifunza kwa wanafunzi wengine.
- Vaa ipasavyo kwa kuvaa sare ya shule au kanuni ya mavazi iliyokubaliwa.
- Tunza mali ya shule na mali ya wafanyakazi na wanafunzi wengine.

Usalama

- Toa mfano na fuata kanuni za shule na za darasa na matarajio kuhusu tabia na mwenendo.
- Kubaliana na tatua migogoro.
- Jihadhari na uchukue jukumu la jinsi tabia na matendo yao yanavyoathiri wengine.
- Jijali mwenyewe na wengine.
- Kuwa salama na kuwasaidia wengine kufanya maamuzi salama ambayo hayawadhuru wao wenyewe au wengine.

Kushiriki

- Fika shuleni na darasani kwa wakati.
- Kuwa tayari kwa kila somo.
- Shiriki kikamilifu katika kujifunza.
- Tamani na jitahidi kupata viwango vya juu katika kujifunza.

Huduma ya mkalimani wa simu

Ikiwa ungetaka taarifa zaidi upige simu mkuu wa shule. Ikiwa unamhitaji mkalimani wa kukusaidia na swali lako, upige simu Huduma ya Mkalimani wa Simu kwa 131 450 na uliza kwa mkalimani katika lugha yako.

Mwambia mpigaji simu ile nambari ya simu unayotaka kupiga na mpigaji wasimu atampata mkalimani kwenye simu ili kukusaidia na mazungumzo. Hutatozwa kwa huduma hii.